

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
SAMPULI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

01

KISWAHILI

MAELEKEZO KWA MSIMAMIZI

Zingatia yafuatayo **kabla ya kusoma maelekezo** kwa watahiniwa:

- (i) Hakikisha unasoma hadithi kwa **sauti** na **taratibu** kwa mara ya kwanza huku ukizingatia alama zote za uandishi zilizopo katika hadithi hiyo. Unaposoma kwa mara ya pili ongeza kidogo kasi ya usomaji.
- (ii) Muda utakaotumika kuwasomea watahiniwa hadithi ni **dakika tano (05)** na muda utakaotumika kwa watahiniwa kujibu maswali ni **dakika tano (05)**. Sehemu hii itafanyika kwa **dakika kumi (10)**.
- (iii) Wakati utakapokuwa unasoma hadithi, hakikisha kuwa watahiniwa hawafungui karatasi yenyeye maswali ya mtihani.
- (iv) Soma kwa sauti maelekezo kwa watahiniwa (1 hadi 4).

MAELEKEZO KWA WATAHINIWA

1. Nitasoma **kwa sauti** hadithi mara mbili, hivyo kila mmoja asikilize kwa makini.
2. Nitakapokuwa nasoma hadithi hakikisha kuwa karatasi yako ya maswali haijafunguliwa.
3. Nikisoma hadithi kwa mara ya kwanza, sikiliza bila kujibu maswali na nikimaliza kusoma kwa mara ya pili, jibu swali la 1 (i) hadi (v) kisha endelea kujibu maswali mengine (2 hadi 6).
4. Naanza kusoma hadithi sasa hivyo **sikiliza kwa umakini**.

HADITHI

Hapo zamani za kale palikuwa na Mfalme aliyeitwa Nguvumali katika nchi ya Hekaheka. Mfalme aliwapenda sana raia. Hata hivyo, Mfalme huyo alikuwa hana raha kwa kuwa alikuwa na siri moyoni. Ukweli ni kwamba, Mfalme alikuwa na masikio kama ya Punda. Hali hii ilimfanya avae kilemba kila siku kinachofunika kichwa na masikio.

Siku moja Mfalme alimuita Roporopo ili amnyoe nywele. Roporopo alipofika alikaribishwa na askari na kuingia katika chumba cha mfalme. Kabla ya kuanza kumnyoa mfalme, aliambiwa na mfalme kuwa atakachoona asiseme popote. Baada ya kumaliza kumnyoa, Roporopo aliondoka na kwenda porini. Alipofika huko alichimba shimo refu kisha akaingia mle na kusema kwa sauti, "Mfalme Nguvumali ana masikio kama ya Punda." Baadaye mti uliota kwenye lile shimo na kurefuka.

Upepo mkali ulipovuma miti ilitikisika. Ndipo ule mti ulitoa maneno kwa sauti kuelekea kijijini, yalisikika maneno yakisema, "Mfalme Nguvumali ana masikio kama ya Punda." Mfalme aliposikia yale maneno alisema, "Ama kweli dunia haina siri." Mwishowe, Mfalme aliamua kuvua kilemba na kukubali watu wajue kuwa ana masikio kama ya Punda.